## MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA MWEZI MEI, 2026 NA MWELEKEO KWA MWEZI JUNI, 2026.

### Dondoo za tathmini ya Mei, 2026 na mwelekeo wa Juni, 2026:

Taarifa hii inatoa muhtasari wa mifumo ya hali ya hewa pamoja na mwenendo wa hali ya hewa kwa mwezi Mei, 2026 na kutoa mwelekeo wa hali ya hewa hususan hali ya joto kwa mwezi Juni, 2026 nchini.


i. Katika kipindi cha mwezi Mei, 2026 baadhi ya maeneo nchini yaliendelea kupata vipindi vya mvua sambamba na vipindi vya mvua kubwa vilivyojitokeza katika maeneo machache.
ii. Mwezi Juni 2026, hali ya joto la chini inatarajiwa kupungua katika maeneo mengi ya nchi ikiashiria kuanza kwa msimu wa Kipupwe (Juni-Agosti), 2026. Aidha, vipindi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache, hususan mwambao wa pwani, ukanda wa Ziwa Victoria na maeneo yenye miinuko ya nyanda za juu kaskazini mashariki.

### 1.0 MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI MEI, 2026.

Katika kipindi cha mwezi Mei, 2026 vipindi vya mvua zilizoamabatana na ngurumo viliendelea kujitokeza katika baadhi ya maeneo nchini, huku ongezeko kidogo la mvua likijitokeza kwenye maeneo machache. Aidha, vipindi vichache vya mvua kubwa na upepo mkali vikijitokeza kwenye maeneo machache. Kiwango cha juu zaidi cha mvua cha milimita 99.7 kilipimwa katika kituo cha hali ya hewa Matangatuani (Kisiwani Pemba) mnamo tarehe 2 Mei, ikifuatiwa na milimita 92.1 katika kituo cha Musoma (mkoa wa Mara) na milimita 69.9 katika kituo cha Lyamungo (mkoa wa Kilimanjaro) mnamo tarehe 5 na 1 Mei, 2026 mtawalia. Vituo vilivyopima mvua milimita 50 au zaidi ni kama inavyoonekana katika kielelezo Namba 1.

Vipindi vya upepo mkali unaofikia au kuzidi kilomita 40 kwa saa vilijitokeza katika baadhi ya maeneo, hususan ukanda wa pwani. Kwa upande mwingine, hali ya baridi ilijitokeza katika maeneo machache, hususan maeneo ya nyanda za juu kusini magharibi. Kiwango cha chini zaidi cha nyuzi joto 7.9 °C kiliripotiwa katika kituo cha Uyole (mkoa wa Mbeya) mnamo tarehe 27 Mei 2026.

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania,
Kiwanja Na. 6, Kitalu “N”, Mtaa wa Fahmida, Dodoma jiji,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz




Kielelezo 1: Vituo vilivyopima viwango vya mvua milimita 50 au zaidi katika mwezi Mei, 2026

## 2.0 MWELEKEO KWA MWEZI JUNI, 2026

### 2.1 MIFUMO YA HALI YA HEWA

Joto la Bahari katika eneo la tropiki ya kati ya Bahari ya Pasifiki linatarajiwa kuwa la juu ya wastani. Joto la bahari katika eneo la magharibi mwa Bahari ya Hindi, karibu na Pwani ya Afrika mashariki, linatarajiwa kuwa la juu ya wastani, wakati eneo la mashariki mwa Bahari ya Hindi linatarajiwa kuwa na joto la bahari la juu kidogo ya wastani. Hali hii inatarajiwa kuongeza upepo wenye unyevu kuvuma kuelekea ukanda wa pwani ya nchi yetu na mikoa ya jirani. Joto la bahari katika eneo la kusini mashariki mwa Bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) linatarajiwa kuwa la chini kidogo ya wastani.

Kwa upande mwingine, joto la bahari katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi (kusini mwa kisiwa cha Madagascar) linatarajiwa kuwa la juu ya wastani. Hali hii inatarajiwa kudhoofisha mgandamizo mkubwa wa hewa (Mascarene) katika eneo hilo na hivyo kupunguza kasi ya upepo wenye baridi kutoka kusini kuelekea katika maeneo ya nchi yetu.

## 2.2 HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI JUNI, 2026

Kipindi cha mwezi Juni 2026, viwango vya joto la chini vinatarajiwa kupungua katika maeneo mengi ya nchi ikiashiria kuanza kwa msimu wa Kipupwe. Hali ya baridi zaidi inatarajiwa kujitokeza katika maeneo ya nyanda za juu Kusini magharibi pamoja na kusini mwa nchi hususan nyakati za usiku na asubuhi.

Aidha, vipindi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache ya ukanda wa pwani, ukanda wa Ziwa Victoria na maeneo yenye miinuko ya nyanda za juu kaskazini mashariki. Kwa upande mwingine, vipindi vichache vya upepo mkali vinatarajiwa kujitokeza katika baadhi ya maeneo, hususan ya ukanda wa pwani na maziwa makuu. Ufuatao ni mwelekeo wa hali ya hewa nchini;

**Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam, kaskazini mwa mkoa wa Morogoro pamoja na visiwa vya Mafia, Unguja na Pemba):**

Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 18 °C hadi 25 °C katika maeneo ya mwambao wa pwani na visiwani. Aidha, katika maeneo ya nchi kavu, viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 12 °C na 20 °C. Vipindi vichache vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache ya mwambao wa pwani.

**Nyanda za juu kaskazini mashariki (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara):**

Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 12 °C hadi 20 °C katika maeneo mengi. Aidha, baadhi ya maeneo ya miinuko yanatarajiwa kuwa na viwango vya chini ya nyuzi joto 12 °C. Kwa ujumla hali ya ukavu inatarajiwa katika maeneo mengi pamoja na vipindi vichache vya mvua hususan katika maeneo ya miinuko.

**Kanda ya Ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Mara na Simiyu):**

Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 14 °C hadi 20 °C katika maeneo mengi. Aidha, maeneo ya miinuko ya mikoa ya Kagera na Geita yanatarajiwa kuwa na kiwango cha chini ya nyuzi joto 14 °C. Kwa upande mwingine, vipindi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache.

**Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora):**

Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 12 °C hadi 20 °C katika maeneo mengi. Aidha, hali ya ukavu kwa ujumla inatarajiwa katika maeneo mengi.

**Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida):**

Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 10 °C hadi 18 °C katika maeneo mengi. Hali ya ukavu inatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi .

**Nyanda za juu kusini magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe, Iringa na kusini mwa mkoa wa Morogoro):**

Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 8 °C hadi 18 °C katika maeneo mengi. Aidha, maeneo ya miinuko (ikijumuisha mkoa wa Njombe) yanatarajiwa kuwa na kiwango cha chini ya nyuzi joto 8 °C. Hali ya ukavu inatarajiwa kujitokeza katika maeneo mengi.

**Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi):**

Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 14 °C hadi 23 °C katika maeneo mengi. Aidha, vipindi vya mvua vinatarajiwa kujitokeza katika maeneo machache ya mwambao wa pwani.

**Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma):**

Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 10 °C hadi 18°C katika maeneo mengi. Maeneo ya miinuko yanatarajiwa kuwa na kiwango chini ya nyuzi joto 10 katika kipindi cha mwezi Juni, 2024. Hali ya ukavu inatarajiwa katika maeneo mengi.

## 2.3 MATARAJIO KWA MWEZI JULY, 2026

Katika kipindi cha mwezi Julai, 2026 hali ya ukavu na baridi inatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi. Aidha, vipindi vya upepo mkali vinatarajiwa kujitokeza katika baadhi ya maeneo.

## 2.4 USHAURI

Tahadhari za kiafya zichukuliwe ili kulinda jamii dhidi ya magonjwa yanayoweza kusababishwa na baridi, vumbi na matumizi ya maji yasiyo safi na salama. Kutokana na

hali ya ukavu inayotarajiwa katika maeneo mengi katika kipindi hiki, maji na malisho yanapaswa kutumika kwa uangalifu ili kupunguza athari zinazoweza kujitokeza.

*Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania inawashauri watumiaji wa taarifa za hali ya hewa ikiwa ni pamoja na wakulima, wafugaji, Mamlaka za Wanyamapori, Mamlaka za Maji na Afya waendelee kutafuta, kupata na kufuata ushauri wa wataalamu katika sekta husika.*

Imetolewa tarehe 01 Juni, 2026 na:

**MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA.**